# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

MKATABA WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA (STAFF HOUSE)

MKATABA NAMBA:

GRRH/001/2021/2022/W/01

KATI YA:

MGANGA MFAWIDHI

HOSPITALI YA RUFAA MKOA,

S.L.P 40,

GEITA

NA

M/S: KELIMO TECH

S.L.P 384

GEITA

APRILI, 2022

# SEHEMU I: FOMU YA MAKUBALIANO YA MKATABA

## Fomu ya Makubaliano ya Mkataba

Makubaliano haya ya Mkataba yanafanywa leo tarehe....11.....mwezi....04...,M*waka 2022* Kati ya **MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA, *S.L.P 40,* GEITA** (Hapa ataitwa "Mwajiri") kwa upande mmoja na **M/S: KELIMO TECH,S.L.P 384,GEITA**. (Hapa ataitwa **MWAJIRIWA**") kwa upande mwingine.

**KWA KUWA:** Mwajiri ana kazi ya MKATABA WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA (STAFF HOUSE), GRRH/001/2021/2022/W/01. hivyo anahitaji FUNDI wa kazi hiyo,

**NA KWA KUWA:** Mwajiriwa yupo tayari kufanya kazi hiyo ya MKATABA WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA (STAFF HOUSE), GRRH/001/2021/2022/W/01.

**HIVYO BASI** mwajiri na mwajiriwa wamekubaliana kuingia katika makubaliano ya mkataba huu kwa masharti yafuatayo;

i. Kwamba, mwajiri atamlipa mwajiriwa kiasi **cha fedha za Kitanzania 14,950,000.00 bila VAT(MILIONI KUMI NA NNE LAKI TISA NA HAMSINI ELFU TU)** ikiwa ni gharama za MKATABA WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA ,GRRH/001/2021/2022/W/01.hadi yakamilike,

ii. Mwajiriwa atatakiwa kufanya kazi hii kwa muda usiozidi miezi miwili (02) tu kuanzia tarehe ya makubaliano haya. Ambayo ni kuanzia tarehe 11 mwezi 04, 2022 hadi tarehe 11 mwezi 06, 2022.

iii. Mwajiriwa atafanya kazi ya MKATABA WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA (STAFF HOUSE), GRRH/001/2021/2022/W/01
_kama ilivyoainishwa kwenye makadirio majenzi na michoro ambavyo ni sehemu ya mkataba huu.

**KATIKA KUSHUHUDIA,** Pande zote mbili zimefanya makubaliano ya Mkataba huu wa MKATABA WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA, GRRH/001/2021/2022/W/01 kama ifuatavyo:

Katika makubaliano haya maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika Masharti ya Mkataba unaorejelewa.

Nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kufasiriwa kuwa ni sehemu ya makubaliano haya, yaani;

1. Fomu ya Makubaliano ya Mkataba;
2. Barua ya Tuzo ya kutunuku kazi.
3. Muhtasari wa Majadiliano
4. Mchanganuo wa bei uliojazwa na fundi
5. Masharti Maalumu ya Mkataba;
6. Masharti ya Jumla ya Mkataba;
7. Michoro;
8. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba.

3. Nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejelewa hapo baadae kama 'Mkataba' na zitachukuliwa kuwa zinakamilisha na zinajieleza sawa iwapo ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyoonyeshwa hapo juu.

4. Katika kuzingatia malipo yanayofanywa na Mwajiri kwa Mwajiriwa kama baadaye inavyotajwa, Mwajiriwa hapa anakubaliana na Mwajiri kutekeleza na kukamilisha kazi kwa kufuata makubaliano, kwa hali zote kulingana na vifungu vya mkataba huu.

Mwajiri hapa anakubali kumlipa Mwajiriwa kwa kuzingatia utekelezaji na ukamilishaji wa kazi, jumla ya **fedha za Kitanzania 14,950,000.00 bila VAT(MILIONI KUMI NA NNE LAKI TISA NA HAMSINI ELFU TU)** kwa ajili ya MKATABA WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA ,GRRH/001/2021/2022/W/01.hadi yakamilike.

**KATIKA KUSHUHUDIA,** pande hizi zimekubaliana na kutia sahihi na muhuri katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

**KATIKA KUSHUHUDIA,** pande hizi zimekubaliana na kutia sahihi na muhuri katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

**KWA NIABA YA MWAJIRI**
**(MGANGA MFAWIDHI GRRH)**

..........................................................

**Sahihi**

(JINA) DKT. MFAUME SALUM

(CHEO)... MGANGA MFAWIDHI

**KWA NIABA YA MWAJIRIWA**
**(FUNDI)** F.muhoja

..........................................................

**Sahihi**

(JINA)... FRANK MUHOJA

(CHEO)... MWEKITI

(Anwani)... 384 GEITA.

KIKUNDI CHA KELIMO TECH
MTAA WA COMPOUND
S.L.P.384-GEITA

**Shahidi/Mbele ya ;**

..........................................................

**Sahihi**

(JINA) DEOGRATIUS MHOJA

(CHEO)... AFISA UGAVI

**Shahidi/ Mbele ya;**

..........................................................

**Sahihi**

(JINA)... JOSEPH FAUSTUS

(CHEO)... KATIBU

(Anwani)... 384 GEITA.

HOSPITALI YA MKOA GEITA
MGANGA MFAWIDHI
S.L.P 40,
GEITA.

## SEHEMU II: BARUA YA KUTUNUKU KAZI.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

MKOA WA GEITA

Anwaniya Simu: "ADMIN"
Simu Nambari:

Nukushi:
Barua pepe: geitarrh@afya.go.tz

HOSPITALI YA RUFAA MKOA,
S.L.P. 40,
**GEITA.**

*Unapojibu tafadhali taja:*
**Kumb. Na. CA.113/133/01/132**

**11 Aprili, 2022**

Kelimo Tech
S.L.P 384
**GEITA**

YAH: **KUTUNUKIWA ZABUNI YA UFUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI (STAFF HOUSE) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA MKOA GEITA- MAGOGO.**
**ZABUNI NA:GRRH/001/2021/2022/W/01**

**SOMO : BARUA YA KUTUNUKU.**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Aidha rejea kazi uliyoomba ya ufundi kwa ajili ya ujenzi wa jingo la Nyumba ya Mganga Mfawidhi katika Hospitali ya Rufaa Mkoa Geita.
GRRH/001/2021/2022/W/01

3. Hii ni kukutaarifu kuwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Geita amekutunuku kazi ya ufundi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Nyumba ya Mganga Mfawidhi (Staff House) Hospitali ya Rufaa Mkoa, GRRH/001/2021/2022/W/01, kwa jumla ya gharama ya fedha za Kitanzania **14,950,000.00 bila VAT (Milioni kumi na Nne laki Tisa na Hamsini Elfu Tu).** Kazi hii ni ya muda wa miezi miwili (02) [Siku 60] tu kuanzia tarehe ya kukabidhiwa eneo la kazi.

4. Nakutakia utekelezaji mwema.

Dkt. Mfaume Salum Kibwana
**MGANGA MFAWIDHI**

HOSPITALI YA MKOA GEITA
MGANGA MFAWIDHI
S.L.P. 40.
GEITA.

KIKUNDI CHA KELIMO TECH
SLP 384
GEITA.
11/04/2022.

KWA
MGANGA MFAWADHI
HOSPITALI YA RUFAA MKOA
SLP 40
GEITA.

**YAH: KUJIBU BARUA YA KUMB NA: CA 113/133/01/129. KIKUNDI CHA KELIMO TECH KIMEKUBALI KUFANYA KAZI YA UJENZI WA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI (STAFF HOUSE KATIKA HOSPITAL YA RUFAA MKOA MAGOGO KWA GHARAMA YA UFUNDI KWA SH. (14,950,000/=) MILIONI KUMI NA NNE NA LAKI TISA NA ELFU, HAMSINI TU.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu kikundi cha kelimo tech kimekubali kufanya kazi ya ujenzi wa nyumba ya Mganga Mfawidhi (Staff house katika hospital ya rufaa Mkoa Magogo kwa gharama ya Sh. (14,950,000/=) milioni kumi na nne na laki tisa na elfu hamsini ambazo ni gharama za ufundi. Vilevile kikundi kiko tayari kwa kufanya kazi hiyo muda wowote kwa spidi ya haraka ili kukamilisha ujenzi huo mapema.

Wako Mkiti wa kikundi cha kelimo tech

F. Mahoji

FRANK MAHOJA.

KIKUNDI CHA KELIMO TECH
MTAA WA COMPOUND
S.L.P 384-GEITA
F.Mahoji

## SEHEMU III: MUHTASARI WA MAJADILIANO.

# KUMBUKUMBU YA MAJADILIANO

**Jina la Taasisi Nunuzi:** HOSPITALI YA RUFAA MKOA-GEITA

**Namba ya Utambulisho ya Zabuni:** GRRH/001/2021/2022/W/01

**Maelezo ya Ununuzi kwa ufupi:** UJENZI WA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI

**Njia ya kufanya Ununuzi:** FORCE ACOUNT (LOCAL FUNDI)

**Tarehe ya majadiliano:** 07/04/2022

**SEHEMU YA 1: KUMBUKUMBU YA MAJADILIANO**

| AGENDA | MAKUBALIANO |
|---|---|
| KUFUNGUA KIKAO | Kikao kilifunguliwa mnamo saa 5:00 asubuhi kwa kutambulishana |
| MDA WA KUMALIZA KAZI | Tulikubaliana muda wa kumaliza kazi yote ni siku 60 (miezi miwili). |
| MALIPO YA AWALI | Tulikubaliana fundi atalipwa na uwezo kwa kazi za awali - Hakuna malipo. |
| KUJADIRI BEI | Tulikubaliana fedha/bei aliyotaja ni sahihi na ipo sawa kutoka kazi yote. |
| MENGINEYO | Fundi aliji[illegible] kuuliza kutumia upatikanaji wa vifaa kwa wakati. - Majibu ni kwamba vifaa vitafika kwa wakati |
| KUFUNGA KIKAO | Kikao kilifungwa mnamo saa 6:30 mchana. |

Tunathibitisha kuwa kumbukumbu za majadiliano tajwa hapo juu ni kweli na sahihi:

| Kwa Taasisi Nunuzi | Kwa Mzabuni |
|---|---|
| Sahihi: [signature] | Sahihi: J. Muhoja [stamp: KIKUNDI CHA KELIMO TECH MTAA WA COMPOUND S.L.P. 384-GEITA] |
| Jina: HIPPOLITUS A. MJIMBE | Jina: FRANK MUHOJA |
| Cheo: MWENYEKITI | Cheo: M/KITI WA KIKUNDI |
| Tarehe: 7/4/2022 | Tarehe: 07/4/2022 |

**Zingatia**: Fomu 14 A and 14B ni viambatinisho kwenye muhtasari

# MAPENDEKEZO YA WAJUMBE WA KAMATI YA MAJADILIANO

*[Kwa ajili ya kuwasilisha kwenye bodi ya zabuni]*

**Jina la Taasisi Nunuzi:** HOSPITALI YA RUFAA MKOA – GEITA
**Namba ya Utambulisho ya Zabuni:** GRRH/001/2021/2022/W/01
**Maelezo ya Ununuzi kwa ufupi:** UJENZI WA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI
**Njia ya kufanya ununuzi:** FORCE ACCOUNT (LOCAL FUNDI)

Kitengo cha Ununuzi (PMU) kinapendekeza majina yafuatayo kwa ajili ya kamati ya Majadiliano kulingana na kanuni ya 226(1) ya Tangazo la Serikali. Na. 446 ya Mwaka 2013.

| Na. | Jina la Mjumbe | Wadhifa/Cheo | Idara | Sababu ya kuchaguliwa *(kwa mfano uelewa wa masuala ya ununuzi/ utaalam/, mwakilishi wa idara tumizi)* |
|---|---|---|---|---|
| 1. | HIPPOLITUS MSIMBE | M/Kiti | OPD | Kiongozi wa OPD pia ni daktari |
| 2. | MASELE WILIAM | Mjumbe | Muuguzi Mfawidhi | Kiongozi katika wauguzi |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Kamati ya majadiliano [*jaza kama/ "ime" au "haija"*] idhinishwa

| Katibu wa Bodi ya Zabuni | Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni |
|---|---|
| Saini: [signature] | Saini: [signature] |
| Jina: Deogratius Mlaja | Jina: DAVID NGOI |
| Tarehe: 08/04/2022 | Tarehe: 08/04/2022 |

# MAOMBI YA KUIDHINISHWA KWA MPANGO WA MAJADILIANO

*[Kwa ajili ya Kuwasilisha kwenye Bodi ya Zabuni]*

**Jina la Taasisi Nunuzi:** HOSPITALI YA RUFAA MKOA – GEITA

**Namba ya Utambulisho ya Zabuni:** GRRH/001/2021/2022/W/01

**Maelezo ya Ununuzi kwa ufupi:** UJENZI WA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI

**Njia ya kufanya ununuzi:** FORCE ACCOUNT (LOCAL FUNDI)

Mpango wa Majadiliano ya zabuni umeandaliwa na kamati ya majadiliano ya zabuni kulingana na kanuni ya 226(6) ya Tangazo la Serikali Na. 446 ya Mwaka 2013.

| Na. | Maeneo ya majadiliano | Madhumuni | Mipaka ya majadiliano |
|---|---|---|---|
| 1. | Muda wa kumaliza ujenzi wa Nyumba | Ni kufikia muafaka katika kukamilisha ujenzi | – Tumekubaliana kujenga kwa muda wa siku 60 kuanzia tarehe ya mkataba |
| 2. | Malipo ya awali katika ujenzi | – Lengo ni kufikia maridhiano katika malipo hayo | – Malipo ya awali hayatakuwepo kwa Fundi |
| 3. | Kujadili Bei ya Koteshen iliyojazwa. | – Kufikia maridhiano ya pande zote mbili | – Bei imebaki kama ilivyo onekana kwenye Koteshen. |
| | | | |
| | | | |

Ninawasilisha Mpango wa Majadiliano ya zabuni kwa ajili ya kuidhinishwa

| **Mwenyekiti wa kamati ya Majadiliano ya zabuni** |
|---|
| Sahihi: [signature] |
| Jina: HIPPOLITUS A. MSIMBE |
| Tarehe: 7/4/2022 |

Mpango wa Majadiliano ya zabuni *[Jaza* neno *"umeidhinishwa" au "haujaidhinishwa"*] kulingana na kanuni ya 227(1) ya tangazo la Serikali Na. 446 ya Mwaka 2013.

| Katibu wa Bodi ya Zabuni | Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni |
|---|---|
| Sahihi: [signature] | Sahihi: [signature] |
| Jina: Dezyntius Mhoji | Jina: DAVID NGOI |
| Tarehe: 08/04/2022 | Tarehe: 08/04/2022 |

## OMBI LA KUIDHINISHA MATOKEO YA MAJADILIANO

*[Kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Bodi ya Zabuni]*

**Jina la Mnunuzi:** HOSPITALI YA RUFAA MKOA - GEITA

**Namba ya Utambulisho ya Zabuni:** GRRH/001/2021/2022/W/01

**Maelezo ya ununuzi kwa ufupi:** UJENZI WA NYUMBA YA MGANGA MFAWIDHI

| | KUMBUKUMBU YA MAJADILIANO | |
|---|---|---|
| **Agenda** | **Makubaliano yaliyofikiwa ( Maelezo Kamili)** | **Yameidhinishwa na Bodi ya Zabuni [andika neno** |
| Mda wa kumaliza ujenzi | | |
| Malipo ya Awali | | |
| ~~Ky~~ Kujadili bei | | |
| | | |
| | | |
| | | |

Taarifa iliyopo katika fomu hii pamoja na nyaraka zilizoambatanishwa ni kamili, za kweli na ni sahihi kulingana na Sheria ya Ununuzi katika Sekta ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 pamoja na kanuni na taratibu zake.

| Katibu wa Bodi ya Zabuni | Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni |
|---|---|
| Sahihi: [signature] | Sahihi: [signature] |
| Jina: Deogratius Mhoji | Jina: DAVID NGOI |
| Tarehe: 08/04/2022 | Tarehe: 08/04/2022 |

**Nyaraka zilizoambatanishwa:** *(orodhesha nyaraka nyingine zote zilizoambatanishwa)*

- Muhtasari wa kikao cha majadiliano

## SEHEMU IV: MCHANGANUO WA BEI ULIOJAZWA NA FUNDI.

KIKUNDI CHA KELIMO TECH
SLP 384
GEITA.

30/03/2022.

KWA:
OFISI YA MGANGA MFAWIDHI MKOA WA GEITA
SLP 40
GEITA.

**YAH: MAOMBI YA UJENZI WA JENGO LA NYUMBA YA WATUMISHI (STAFF HOUSE) HOSPITAL YA RUFAA YA MKOA WA GEITA. JUMLA YA GHARAMA YA UFUNDI NI SH: 14,950,000/= MILIONI KUMI NA NNE NA LAKI TISA NA ELFU HAMSINI TU.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu Kikundi cha Kelimo tech kinaomba kazi ya ujenzi wa jengo la nyumba ya watumishi (staff House) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita kwa gharama ya sh. 14,950,000/= ambayo ni gharama ya ufundi. Sisi kama Wanakikundi cha Kelimo tech tuna uzoefu wa kazi za ufundi ujenzi na nimafundi stadi na weledi na wenye kuzingatia Mkataba. Kutokana na hilo baadhi ya Sehemu tulizofanya ni Ujenzi wa vyumba (6) vya Madarasa S/msingi Uwanja Kalike Halmashauri ya Mji Geita, Nyumba (2) za wakuu wa Idara Magogo Geita, Pia tumejenga jengo la, choo cha Msufini Halmashauri ya Mji Geita, Pia tumefanya umaliziaji wa Majengo ya GPSA ofisi Geita. Hizo kazi zote tajwa hapo juu zimefanyika na kukamilika kwa wakati.

NB. Kutokana na hilo nimeambatanishe nakala za baadhi ya mikataba ya Majengo tuliyojenga, vile vile nimeambatanisha na nakala ya Bank statement, Usajili wa Kikundi nk.

Tutashukuru Iwapo Ombi letu litakubaliwa

Wako Mtiifu
Mkiti wa kikundi cha Kelimo tech
F. Muhoja
FRANK MUHOJA RAYMOND

Tell. 0621633060
2. 0745735195.

KIKUNDI CHA KELIMO TECH
MTAA WA COMPOUND
S.L.P. 384-GEITA.
Muhoja

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA GEITA
UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI
GHARAMA ZA UFUNDI

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - Shs |
|---|---|---|
| A | **Msingi wa Jengo (Sub-structure)** | |
| 1 | Kusafisha eneo | 200,000/= |
| 2 | kuset jengo | 150,000/= |
| 3 | Uchimbaji wa msingi | 250,000/= |
| 4 | ziada kuchimba msingi kwenye mwamba | 400,000/= |
| 5 | Kujaza kifusi kwenye msingi | 300,000/= |
| | | |
| | **Formwork** | |
| 4 | Pembezoni mwa jamvi | 150,000/= |
| 5 | Pembezoni mwa nguzo | 100,000/= |
| 6 | Kuondoa formwork | 100,000/= |
| | | |
| | **Kumwaga zege** | |
| 7 | Chini kwenye msingi wa tofali | 250,000/= |
| 8 | Chini kwenye msingi wa nguzo | 100,000/= |
| 9 | katika nguzo ya awali | 150,000/= |
| 10 | kwenye jamvi | 300,000/= |
| 11 | Ujenzi wa tofali (1200) | ~~900,000/=~~ x 540,000/= F.Mhoji |
| | | |
| | **Mawe** | |
| 12 | Upangaji wa mawe,kuweka mchanga na dawa ya mchwa na utandazaji wa DPM | 300,000 |
| | | |
| 13 | Umwagiliaji wa maji | 150,000/= |
| | **Jumla ndogo msingi wa jengo** | ~~3,400,000/=~~ x 3,440,000/= F.Mhoji |
| | | |
| B. | **Kunyanyua jengo (Super-structure)** | |
| 1 | Ujenzi wa tofali za kuta (23000) na uwekaji DPC | ~~1,500,000/=~~ x 1,150,000/= F.Mhoji |
| | | |
| | **Kufunga formwork katika:** | |
| 2 | Nguzo mlalo | 200,000/= |
| 3 | Nguzo wima | ~~100,000/=~~ x 50,000/= F.Mhoji |
| | | |
| | **Kusuka nondo katika:** | |
| 4 | Nguzo mlalo | 200,000/= |
| 5 | Nguzo wima | ~~150,000/=~~ x 50,000/= F.Mhoji |
| | | |
| | **Kumwaga zege katika:** | |
| 6 | Nguzo mlalo | 200,000/= |
| 7 | Nguzo wima | 50000/= |
| 8 | Umwagiliaji wa maji | 200,000/= |
| | JUMLA NDOGO KUNYANYUA JENGO | ~~2,600,000/=~~ x 2,100,000/= F.Mhoji |
| C. | **Kuezeka (Roof structure and covering)** | |
| | Kuezeka na ufungaji wa gata | 1300,000/= |
| | **Jumla ndogo kunyanyua jengo** | 1,300,000/= |

F.Mhoji

KIKUNDI CHA KELIMO TECH
MTAA WA COMPOUND
S.L.P. 384-GEITA

| | MAJUMUISHO (SUMMARY) | |
|---|---|---|
| | | |
| A. | Msingi wa Jengo (Sub-structure) | ~~3,400,000/=~~ x 3,440,000/= F.mihogo |
| | | |
| B. | Kunyanyua jengo (Super-structure) | ~~2,600,000/=~~ x 2,100,000/= F.mihogo |
| | | |
| C. | Kuezeka (Roof structure and covering) | 1,300,000/= |
| | | |
| D. | Milango | |
| | | |
| E. | Umaliziaji (Finishing) | 4,000,000/= |
| | | |
| F. | Rangi na Mapambo (Painting & Decoration) | 1,150,000/= |
| | | |
| G. | Umeme (Electrical installation) | ~~500,000/=~~ x 960,000/= F.mihogo |
| H. | Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system) | 2,000,000/= |
| | | |
| | **JUMLA KUU Shs.** | 14,950,000/= |
| | | |
| | **ANGALIZO:** | |
| | | |
| | Fundi anatakiwa kujaza hii fomu kwa kupitia mchoro wa jengo husika | |

F.mihogo

KIKUNDI CHA KELMO TECH
MTAAWA COMPOUND
S.L.P.384-GEITA

## SEHEMU V: MASHARITI MAALUMU YA MKATABA.

**Mashariti Maalumu ya Mkataba.**

Taarifa maalumu ifuatayo kwa ajili ya kazi inayofanywa itakuwa nyongeza, au inaweza kurekebisha vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba. Kunapokuwa na mgogoro, vifungu katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** vitakuwa na nguvu zaidi ya vifungu katika **Masharti ya Jumla ya Mkataba**.

| **Masharti Maalumu ya Mkataba Kifungu Na.** | **Masharti ya Jumla ya Mkataba Kifungu Na** | **Marekebisho ya, na Nyongeza kwa vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba.** |
|---|---|---|
| **1** | **20.0** | Mkataba utaanza tarehe: 11 mwezi 04,2022 hadi tarehe 11, mwezi 06,2022. |
| **2** | **20.0** | Muda wa kukamilisha kazi: Miezi miwili (02), |
| **3** | **23.1** | Malipo ya awali: Hakuna. |
| **4** | **23.2** | Fundi atatakiwa kulipa tozo za makato kwa mamlaka husika kwenye Mkoa. |
| **5** | **23.4** | Kiwango cha riba kwa kiasi kisicholipwa ni kile kiwango cha riba kwa mwezi kinachotumiwa na benki ya biashara kama kilivyopitishwa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe ya kutia sahihi mkataba. |
| **6** | **26.0** | Kiasi cha kulipia ucheleweshaji kazi: ***0.1% ya kiasi cha Mkataba*** kwa siku na isizidi 10% ya Kiasi cha Mkataba |

## SEHEMU VI: MASHARITI YA JUMLA YA MKATABA.

## A: VIFUNGU JUMLA

### Kifungu 1: Nyaraka za Mkataba

Masharti ya Mkataba na fomu ya Maelezo ya mahitaji, Viwango na vipimo ni sehemu muhimu ya nyaraka za Mkataba na zinapaswa kusomwa pamoja na nyaraka nyingine zote zinazounda Mkataba. Kama ikitokea kunaonekana kuna mgogoro kipaumbele cha nyaraka kitakuwa kama ilivyoainishwa katika **Kifungu cha 6** cha Masharti ya Mkataba.

### Kifungu 2: Tafsiri

Katika haya Masharti ya Mkataba, maneno yafuatayo yatakuwa na maana zilizotolewa kwa maneno hayo kama ilivyo hapa chini:

**Mwajiri:** ***Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa-Geita.***

**Mhandisi wa mkoa :**Mtu aliyeteuliwa na Mwajiri na kuwa na wajibu wa usimamizi wa kazi na usimamizi wa mkataba

**Mwakilishi wa Mhandisi:** Mtu aliyeteuliwa na Mhandisi mwenye wajibu wa Kusimamia Kazi.

**Mkandarasi/Local Fundi :**Mtu au watu au kampuni ambayo zabuni yao imekubaliwa na Mwajiri.

**Kazi: Ni** Kazi zinazotakiwa kufanywa kulingana na mkataba.

### Kifungu 3: Maelekezo

Maelekezo yanayotolewa na Mhandisi yatakuwa kwa maandishi. Ikiwa kwa sababu nyingine yoyote ile maelekezo hayo yakatolewa kwa mdomo, Mkandarasi/Local fundi atafuata maelekezo hayo. Katika kipindi cha **siku 7** maelekezo hayo ya mdomo yatathibitishwa kwa maandishi .

### Kifungu 4: Lugha

Notisi zote, maelekezo na mawasiliano au waraka wowote wa maandishi unaohusu mkataba utakuwa kwa Kiswahili kadri itakavyokubaliwa na pande zote ilimradi, nyaraka zote zinazotolewa kuhusiana na mkataba unaotekelezwa kwa ushirikiano wa fedha za mkopo au ruzuku

zitaandikwa kwa Kiingereza/kiswahili

**Kifungu 5: Sheria inayotumika**

Mkataba, maana yake, fasiri yake, na utekelezaji wake vitaongozwa na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Kifungu 6: Nyaraka za Mkataba zenye Kipaumbele**

Nyaraka kadhaa zinazofanya mkataba zichukuliwe kuwa zinajieleza kikamilifu lakini kama ikitokea hitilafu yoyote ile nyaraka zenye umuhimu wa kwanza zitakuwa zifuatazo:

1. Fomu ya Makubaliano ya Mkataba;
2. Barua ya Tuzo ya kazi
3. Muhtasari wa Majadiliano
4. Mchanganuo ulizojazwa na Fundi
5. Masharti Maalumu ya Mkataba;
6. Masharti ya Jumla ya Mkataba;
7. Michoro;
8. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba

**B: MAJUKUMU**

**Q1`Kifungu 7: Utekelezaji wa Kazi**

Fundi, atatoa nguvu kazi na zana zakufanyia kazi, vifaa na cho chote kile kinachohitajika kwa ukamilishaji wa kazi ikiwa ni pamoja na maji na umeme vitatolewa na Mwajiri. Atafanya kazi kulingana na inavyotakiwa na nyaraka za mkataba, na maelekezo ya ziada kama yatakavyotolewa mara kwa mara.

**Kifungu 8: Hali Mbaya ya Ukinzani**

Iwapo wakati wa utekelezaji wa kazi Mkandarasi/Local fundi atapambana na hali mbaya ya ukinzani ambayo haihusiani na hali ya hewa na ambayo haikuwa imetabiriwa na Mkandarasi/Local fundi, Mhandisi atatathimini kuongeza muda ambao Mkandarasi/Local fundi, anastahili.

**Kifungu 9: Kutoa kazi kwa Mkandarasi Msaidizi**

Mkandarasi /Local fundi, hatatoa kazi au sehemu ya kazi kwa Mkandarasi /Local fundi, msaidizi kibali cha maandishi cha kutoka kwa Mwajiri. Kibali kama hicho kinapotolewa hakimwondolei Mkandarasi/Local fundi mamlaka au majukumu yake chini ya maktaba na hivyo Mkandarasi atakuwa na wajibu kwa kushindwa au kuzembea kwa Wakandarasi wasaidizi.

**Kifungu 10: Usimamizi wa Kazi Unaofanywa na Mkandarasi**

Mkandarasi/fundi atatekeleza kazi kwa uangalifu na kwa kufuata utendaji unaotakiwa na Mhandisi ili kufikia mahitaji maalumu ya ubora, kiasi na muda uliopangwa. Kama katika wakati wowote ule Mhandisi anaona uzembe, au kubadilika sana kwa mwelekeo wa programu, hatua zinazofaa zitachukuliwa na Mkandarasi ili kurekebisha hali.

**Kifungu 11: Ukaguzi**

Mhandisi au mwakilishi wake aliyempa mamlaka ana haki ya kukagua kazi na Mkandarasi atatoa usaidizi kwa shughuli hiyo na kwa wakati Mhandisi atakapohitaji.

**Kifungu 12: Kazi Zinazokataliwa**

Kazi ambazo hazikuzingatia masharti ya mkataba zitakataliwa. Kwa maelekezo ya Mhandisi, Mkandarasi/Local fundi kwa gharama zake mwenyewe atatengeneza au kurekebisha au kufanya upya kazi itakayokataliwa hadi kumridhisha Mhandisi.

**Kifungu 13: Bima**

Mkandarasi/Local fundi ataweka bima yenye jina lake na Mwajiri kwa ajili ya hasara au uharibifu wa zana, vifaa na mitambo ya Mkandarasi na pia kwa kufidia majeruhi au vifo.

**Kifungu14: Wajibu wa Mkandarasi**

Mkandarasi hatamhusisha Mwajiri dhidi ya madai yoyote yanayotokana na hasara au uharibifu wa upande wa tatu (third party). Atamkinga kikamilifu Mwajiri wake dhidi ya madai au hasara zitakazotokana na Sheria ya Ajira na Fidia ya Wafanyakazi.

**Kifungu15: Jambo Lisilozuilika**

Katika tukio la hasara yoyote au uharibifu unaotokea katika utendaji wa aina yoyote wa nguvu za asili ambao pande za mkataba hazikuweza kufikiria mapema, Mkandarasi/Local fundi atarekebisha hasara au uharibifu. Mwajiri ataaamua kutoa ziada ya Bei ya Mkataba na pia anaweza kufikiria kutoa muda wa nyongeza wa kipindi cha mkataba.

**Kifungu16: Ubora wa Maunzi na Usanifu wa Kazi**

Maunzi yote na usanifu wa kazi vitakuwa na ubora kama ilivyofafanuliwa

katika mkataba na pia kulingana na maelekezo ya Mhandisi na vitapimwa kama Mhandisi atakavyoona inafaa. Mkandarasi atatoa bure msaada unaohitajika kwa ajili ya kupima ubora wa maunzi na atakuwa na wajibu wa kugharimia upimaji wote utakaohitajika.

**Kifungu 17: Upatikanaji wa Maunzi**

Mkandarasi/Local fundi atabainisha vyanzo vyote vya maunzi yanavyohitajika kabla ya kuanza kwa kazi. Mwajiri akitakiwa anaweza kuwezesha upatikanaji wa vyanzo hivyo. Mkandarasi/Local fundi hatatumia maunzi bila kwanza kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mhandisi.

**Kifungu18: Usafishaji wa Eneo la Kazi**

Baada ya kumaliza kazi, Mkandarasi/Local fundi ataondoa kutoka eneo la kazi zana zote, na maunzi ya ziada, uchafu na mitambo ya muda na ataacha eneo la kazi likiwa safi na katika hali itakayokubaliwa na Mhandisi.

**Kifungu19: Afya, Usalama na Kulinda Mazingira.**

Mkandarasi/Local fundi katika kipindi chote cha mkataba atakuwa na wajibu kamili ya kiafya na kiusalama katika eneo lake ya kazi na watu wote wanaopaswa kuwa katika eneo la kazi katika hali ya mpango mzuri ili kuepusha hatari kwa watu hao.

Mkandarasi/Local fundi atazingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira kama zinavyoelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Kifungu20: Kuanza na Kukamilika kwa Kazi.**

Mkandarasi/Local fundi ataanza na kukamilisha kazi katika muda ulioelezwa kwenye Masharti Maalumu ya Mkataba au katika kipindi cha mkataba cha nyongeza, kama kipindi hicho kimeruhusiwa na Mwajiri.

**Kifungu21: Mabadiliko ya Wigo wa kazi**

Kwa idhini ya Mwajiri, Mhandisi anaweza kubadilisha umbo, ubora au kiasi cha kazi na atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Mkandarasi/Local fundi ipasavyo. Mabadiliko hayo yatafanywa kwa agizo la Mabadiliko katika Mkataba. Mhandisi ataamua kuhusu kiasi (kama itatokea) ambacho kwa maoni yake kinapaswa kuongezwa au kupunguzwa kutoka jumla ya fedha iliyotajwa kwenye Mkataba kwa ajili ya kazi yoyote ya nyongeza iliyofanywa au iliyoachwa kwa agizo hilo. Kiasi cha fedha kitakachoamuliwa kitatokana na kiwango cha kizio au kama hakuna

na matengenezo yote kama yapo yatakuwa yametekelezwa na hivyo mhandisi kuridhika.

### 23.4 Ucheleweshwaji wa Malipo

Kama mwajiri atashindwa kufanya malipo katika muda uliotajwa, Mwajiri atamlipa Mkandarasi/Local fundi riba katika kiwango kilichotajwa kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba**.

### 23.5 Makato ya Malipo

Mwajiri atakuwa na haki ya kukata fedha kiasi cho chote, fedha ya advansi au madeni yanayolipika kutoka kwa Mkandarasi/Local fundi kwenda kwa Mwajiri kutokana na fedha yoyote anayoweza kulipwa Mkandarasi/Local fundi na Mwajiri chini ya mkataba huu au mkataba mwingine ilimradi kifungu hiki hakitaathiri marekebisho yoyote kwa amri ya sheria au pengine Mwajiri anaweza kuwa na haki ya kurudishiwa fedha yoyote kama hiyo.

### 23.6 Malipo kwa Wafanyakazi

Kama kutatokea kushindwa kulipa mishahara/ujira na fidia nyingine zinazopaswa kulipwa wafanyakazi na /au malipo ya kukodisha mitambo/zana/magari na vifaa chini ya mkataba huu, mwajiri atakuwa na haki ya kushikilia malipo ya Mkandarasi /Local fundi.
Mwajiri atatumia fedha alizoshikilia kuwalipa wafanyakazi wa Mkandarasi/Local fundi mishahara yao na fidia nyingine na ada za kukodisha maunzi. Malipo kama hayo yatachukuliwa kuwa ni malipo yaliyopokelewa na Mkandarasi/Local fundi kutoka kwa Mwajiri chini ya mkataba huu.

## 24: Malipo ya Ucheleweshaji kazi

Kama Mkandarasi /Local fundi atashindwa kukamilisha kazi yake katika muda uliotajwa kwenye mkataba au katika muda wowote wa nyongeza ulioruhusiwa na Mwajiri, Mkandarasi /Local fundi atamlipa Mwajiri malipo ya ucheleweshaji wa kazi katika kiwango cha asilimia 0.1 cha thamani ya mkataba kwa siku mpaka kiwango cha juu cha asilimia 10 ya bei ya mkataba

kiwango cha kizio kinachotumika, kiwango kingine kitatumika kama itakavyoamriwa na Mhandisi na kukubaliwa na wote, Mwajiri na Mkandarasi.

## C: MALIPO

### Kifungu 22: Kiasi

Kiasi kilichowekwa kwenye mchanganuo wa Makadirio ya Kazi ni kiasi kilichokadiriwa kwa kazi na kisichukuliwe kuwa ndiyo kiasi halisi sahihi kitakachofanywa na Mkandarasi.

Mhandisi atapima thamani ya kazi halisi iliyofanyika na ataidhinisha gharama halisi ya kazi iliyofanyika kama ilivyofafanuliwa katika mkataba. Ukomo wa kiasi cha kazi unaweza kuongezeka au kupungua kwa asilimia 10 ya bei ya mkataba na hii haitahitaji kibali cha Bodi ya Zabuni.

### Kifungu 23: Malipo

#### 23.1 Malipo ya Awali

Malipo ya Awali ya **asilimia 15** ya thamani ya mkataba **yanaweza** kutolewa kama itakuwa inaonyesha hivyo kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba** baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali inayokubalika. Malipo ya awali yatakatwa kwa mafungu katika madai yatakayowasilishwa na Mkandarasi /Local fundi kwa malipo, mpaka malipo ya awali yote yatakaporudishwa kikamilifu.

#### 23.2 Malipo Wakati Kazi Inaendelea

Malipo yatafanywa kwa Mkandarasi /Local fundi wakati kazi inaendelea baada ya Mhandisi kutoa cheti kinachoonyesha kuwa kazi imekamilika kwa viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba. Katika kila cheti mwajiri atashikilia kiasi kilichotajwa katika Masharti Maalum ya Mkataba na kisichozidi asilimia kumi ya bei mkataba. Fedha hiyo iliyoshikiliwa italipwa katika cheti cha malipo ya mwisho.

Kiasi cha fedha anachodai Mkandarasi /Local fundi kitalipwa na Mwajiri kwa Mkandarasi /Local fundi katika kipindi ndani ya **siku 14 za kazi** baada ya idhini ya cheti cha malipo kutolewa na Mhandisi.

#### 23.3 Malipo ya Mwisho

Cheti cha malipo ya mwisho kitatolewa ndani ya siku **28** za kazi baada ya nyaraka hiyo kuidhinishwa na Mwajiri, ilimradi kazi zote, marekebisho yote

na matengenezo yote kama yapo yatakuwa yametekelezwa na hivyo mhandisi kuridhika.

### 23.4 Ucheleweshwaji wa Malipo

Kama mwajiri atashindwa kufanya malipo katika muda uliotajwa, Mwajiri atamlipa Mkandarasi/Local fundi riba katika kiwango kilichotajwa kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba**.

### 23.5 Makato ya Malipo

Mwajiri atakuwa na haki ya kukata fedha kiasi cho chote, fedha ya advansi au madeni yanayolipika kutoka kwa Mkandarasi/Local fundi kwenda kwa Mwajiri kutokana na fedha yoyote anayoweza kulipwa Mkandarasi/Local fundi na Mwajiri chini ya mkataba huu au mkataba mwingine ilimradi kifungu hiki hakitaathiri marekebisho yoyote kwa amri ya sheria au pengine Mwajiri anaweza kuwa na haki ya kurudishiwa fedha yoyote kama hiyo.

### 23.6 Malipo kwa Wafanyakazi

Kama kutatokea kushindwa kulipa mishahara/ujira na fidia nyingine zinazopaswa kulipwa wafanyakazi na /au malipo ya kukodisha mitambo/zana/magari na vifaa chini ya mkataba huu, mwajiri atakuwa na haki ya kushikilia malipo ya Mkandarasi /Local fundi.
Mwajiri atatumia fedha alizoshikilia kuwalipa wafanyakazi wa Mkandarasi/Local fundi mishahara yao na fidia nyingine na ada za kukodisha maunzi. Malipo kama hayo yatachukuliwa kuwa ni malipo yaliyopokelewa na Mkandarasi/Local fundi kutoka kwa Mwajiri chini ya mkataba huu.

## 24: Malipo ya Ucheleweshaji kazi

Kama Mkandarasi /Local fundi atashindwa kukamilisha kazi yake katika muda uliotajwa kwenye mkataba au katika muda wowote wa nyongeza ulioruhusiwa na Mwajiri, Mkandarasi /Local fundi atamlipa Mwajiri malipo ya ucheleweshaji wa kazi katika kiwango cha asilimia 0.1 cha thamani ya mkataba kwa siku mpaka kiwango cha juu cha asilimia 10 ya bei ya mkataba

## D: KUSULUHISHA MIGOGORO NA KUVUNJA MKATABA

### Kifungu 25: Kusuluhisha Migogoro

Kama migogoro ikitokea itasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote. Kama mazungumzo yatashindwa kuleta makubaliano, kila upande una hiari ya kwenda kwenye maamuzi kulingana na sheria za Tanzania.

### Kifungu 26: Uvunjaji wa Mkataba

26.1 Kama Mkandarasi/Local fundi anashindwa kuanza kazi katika muda uliopangwa au kuna sababu ya kutosha kuwa hatakamilisha kazi katika muda uliopangwa au kuna ucheleweshaji uliokiuka tarehe ya kukamilisha kazi au hayuko makini kufuata maelekezo yanayotolewa na Mhandis/Local fundi au anakuwa mufilisi, Mwajiri atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kumwajiri Mkandarasi/Local fundi mwingine kufanya kazi hiyo.

26.2 Kama Mwajiri atashindwa kumlipa Mkandarasi/Local fundi katika muda wa siku 30 tangu tarehe ya cheti cha malipo kuidhinishwa na Mhandisi, Mkandarasi/Local fundi anaweza kuvunja mkataba.

### Kifungu 27: Malipo kama Mkataba Umevunjwa

Kama mkataba utavunjwa, Mkandarasi/Local fundi atalipwa na Mwajiri kiasi cha fedha au vifaa ambavyo havitakuwa tayari vimelipiwa katika malipo yaliyofanywa kwa Mkandarasi/Local fundi kwa kazi zote zilizofanywa kabla ya tarehe ya kuvunjwa kwa mkataba kwa kiwango na bei inayotolewa kwenye mkataba. Kila malipo yoyote yanayofanywa na Mwajiri chini ya kifungu hiki, mwajiri atakuwa na haki ya kulipwa madeni yote kutokana na malipo ya awali aliyolipwa Mkandarasi/Local fundi kwa ajili ya kazi hii na jumla yote ya fedha ambayo imelipwa hapo awali na Mwajiri kwenda kwa Mkandarasi/Local fundi kwa minajiri ya utekelezaji wa kazi.